MWONGOZO KAMILI WA NDOA YA KIISLAMU

UCHUMBA, NDOA, TALAKA, KUNYONYESHA

SEHEMU YA KWANZA

IMEANDALIWA NA

ABUU ZAKARIYYAA, YAHYA HASSAN ALHANBALY

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Kila sifa njema ni stahiki ya Allah, Mola Mlezi wa Viumbe Wote. Mola Mlezi ambaye ameumba jinsia mbili - ya kiume na ya kike, na akajaalia kupitia jinsia hizi mbili, kubakia kizazi cha wanaadamu na wanyama.

Sala na Salamu zimfikie Mtume wa Mwisho, Muhammad na Wafuasi wake mpaka siku ya mwisho.

Hii ni Makala ya kwanza katika mfululizo wa makala zinazofunamana na maudhui ya ndoa. Nimekusudia kuandika makala fupi zinazogusa sehemu ya maudhui ya ndoa kuanzia hatua ya uchumba, maisha ya ndoa, talaka, eda na kunyonyesha mtoto.

Katika makala hii, nitaangazia mambo yafuatayo:-

1. Maana ya ndoa kisheria
2. Mahimizo ya kuiendea ndoa
3. Hekima ya kuwekwa sheria ya ndoa
4. Hukumu ya kisheria ya kuoa au kuolewa
5. Idadi ya wake anaoruhusiwa mwanaume kuoa
6. Nasaha kwa wasimamizi wa vijana wa kike na kiume

MAANA YA NDOA KISHERIA

وشرعاً: عقد يتضمن إباحة استمتاع كل من الزوجين بالآخر، على الوجه المشروع

"(Ndoa) kisheria ni mafungamano (baina ya mwanaume na mwanamke) ambayo hufaa kila mmoja katika wanandoa kustarehe na mwenza wake katika namna inayofaa kisheria"[1]

MAHIMIZO YA KUIENDEA NDOA

Sheria ya kiislamu imehimiza sana kila mwenye uwezo wa kuoa, aingie katika ndoa. Amesema Allah ﷻ

﴿ فَٱنكِحُواْ مَا طَابَ لَكُم مِّنَ ٱلنِّسَآءِ مَثۡنَىٰ وَثُلَٰثَ وَرُبَٰعَۖ فَإِنۡ خِفۡتُمۡ أَلَّا تَعۡدِلُواْ فَوَٰحِدَةً أَوۡ مَا مَلَكَتۡ أَيۡمَٰنُكُمۡۚ ذَٰلِكَ أَدۡنَىٰٓ أَلَّا تَعُولُواْ ۝٣ ﴾

النساء [٣]

Basi oeni wanaopendeza kwenu katika wanawake, wawili wawili, watatu watatu, wanne wanne. Na endapo mkihofia kutowafanyia uadilifu basi oeni mmoja. (Suurat Annisaa, aya 3)

Vilevile Mtume wetu Muhammad ﷺ amehimiza kundi la vijana kuingia katika ndoa. Kundi ambalo ndilo lenye kuleta uharibifu lau si kama kuhimizwa kuingia katika

[1] Al-fiqhul-muyassar uk.269

ndoa. Na ndio kundi ambalo ndani yake hupatikana matunda ya ndoa – watoto wengi.

عَنْ عَبْدِ اللهِ قَالَ: ((قَالَ لَنَا رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ، مَنِ اسْتَطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ، فَإِنَّهُ أَغَضُّ لِلْبَصَرِ، وَأَحْصَنُ لِلْفَرْجِ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصَّوْمِ، فَإِنَّهُ لَهُ وِجَاءٌ))

Kutoka kwa Abdullah amesema, “Amesema Kutuambia sisi Mjumbe wa Allah – Sala na Salamu zimfikie: Enyi kongamano la vijana! Yeyote atakayeweza miongoni mwenu gharama za ndoa, basi aoe. Hakika ndoa inashusha zaidi macho, na inahifadhi zaidi utupu. Na asiyeweza (kuoa) basi alazimiane na funga, kwani funga ni kinga kwake”[2]

Na pia Mtume ﷺ hakuchelea kukemea watu kujitenga na ndoa

عن سَعْدَ بْنَ أَبِي وَقَّاصٍ يَقُولُ: رَدَّ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَلَى عُثْمَانَ بْنِ مَظْعُونٍ التَّبَتُّلَ، وَلَوْ أَذِنَ لَهُ لَاخْتَصَيْنَا

Kutoka kwa Sa’ad ibn Abii Waqqaas amesema, “Mjumbe wa Allah ﷺ alimkatalia U’thman ibn Madh’un kujitenga na ndoa na kujikita katika ibada. Na lau Mtume – Juu yake Sala na Salamu- angempa idhini tungeziharibu korodani zetu. [3]

Na nyinginezo katika dalili zilizokuja kuhimiza kuiendea ndoa. Zote hizo ni dalili tosha ya kuwa sheria ya kiislam imelipa kipaumbele jambo la ndoa.

Basi ni jambo la kustaajabisha kwa vijana leo hii ambao wanahofia kuingia katika ndoa kwa visingizio mbalimbali, tena visivyokuwa na mashiko, ilihali wanaendelea kumuasi Allah kwa kufanya uzinifu. Na wengine wao sababu yao ni kuwa wanajipanga kimaisha. Na wengine mpaka wawe na maisha ya hadhi ya juu. Tambua ya kwamba ewe kijana! Ikiwa wahitaji maisha mazuri, basi harakia kuingia katika ndoa. Anasema Allah ﷻ

﴿ وَأَنكِحُواْ ٱلۡأَيَـٰمَىٰ مِنكُمۡ وَٱلصَّـٰلِحِينَ مِنۡ عِبَادِكُمۡ وَإِمَآئِكُمۡۚ إِن يَكُونُواْ فُقَرَآءَ يُغۡنِهِمُ ٱللَّهُ مِن فَضۡلِهِۦۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٞ ٣٢ ﴾

النور [٣٢]

Na waozesheni wasio na wenza (mke au mume) miongoni mwenu - wema katika watumwa na vijakazi wenu. Ikiwa watakuwa mafukara, Allah atawatajirsha kwa fadhila zake. Na Allah ni mwenye wasaa, mwenye elimu (Suurat nuur, aya 32)

[2] Sahihi Muslim, Hadithi na. 4000
[3] Sahihi Bukhari, hadithi na. 4786

HEKIMA YA KUWEKWA SHERIA YA NDOA

Kuna hekima nyingi zinazofungamana na kuwekwa kwa sheria ya ndoa katika uislam. Miongoni mwa hekima hizo ni[4]:-

1. Kuendelea kwa kizazi cha mwanadamu. Lau isingelikuwa kuoana na kuzaliana, basi kizazi cha Adam kisingekuwepo na kingetoweka.
2. Kuuhifadhi utupu kutokana na kustarehe katika sehemu isiyo halali kwake, ambapo kufanya hivyo - kustarehe sehemu isiyo ya halali, ni sababu ya kuharibika kwa maadili ya jamii.
3. Kupatikana utofauti baina ya maisha ya wanaadamu na maisha ya wanyama, kwa kukiinua kizazi cha mwanadamu kuwa chenye thamani zaidi ya wanyama.
4. Kuhifadhi nasabu na kupatikana mafungamano ya ndugu baina yao.
5. Kupatikana utulivu, maliwazo, na kustarehe baina ya wanandoa

﴿وَمِنْ ءَايَٰتِهِۦٓ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَٰجًا لِّتَسْكُنُوٓا۟ إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾﴾ الروم [٢١]

Na miongoni mwa alama za kuwepo Allah, ni kukuumbieni kutokana na nafsi zenu wake, ili mpate kutulizana kwao, na akajaalia baina ya wanandoa mapenzi na huruma. Hakika katika hilo kuna ishara tosha kwa wenye kutafakari. (Suurat Ar-ruum, aya ya 21)

﴿ * هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَٰحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا ۖ﴾ الأعراف [١٨٩]

Yeye (Allah) amekuumbeni kutokana na nafsi moja (Adam) na akaumba kutoka na nafsi hiyo mkewe ili apate kutulizana kwake.
(Suurat Al-a’araaf, aya 189)

6. Mwanaume kumsimamia mwanamke kwa kumuongoza katika ya sawa na kumuepusha na ya batili, na kumsimamia matumizi yake

﴿ ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ﴾ النساء [٣٤]

Wanaume ni wasimamizi wa wanawake, kwasababu ya Allah kuwafadhilisha baadhi yao kwa wengine na kwa kile wanachokitoa (wanaume) katika mali zao.
(Suurat Annisaa, aya 34)

[4] Angalia kitabu Al-mulakhasul-fighiy 2/322 cha Sheikh Fawzaan Al-fawzaan

HUKUMU YA KISHERIA YA KUOA AU KUOLEWA

Hukumu ya kisheria ya kuoa au kuolewa inategemea hali ya mtu mmoja na mwingine, kama ifuatavyo[5]:-

1. **Wajibu (Lazima kwake ndoa):** kwa mwenye kuhofia zinaa endapo asipoingia katika ndoa. Kwake ndoa na inakuwa ni bora kulikoni hajji, swala na swaumu za sunna. Na hii hukumu haitegemei baina ya aliye na uwezo wa kuhudumia au la, bali inabidi afanye utaratibu wa kuliingia jambo la ndoa na Allah atamfungulia riziki kwa fadhila zake
2. **Sunna/ mustahabu (Inapendelewa kwake ndoa):** ni kwa yule ambaye ana matamanio na hana hofu ya kufanya uzinifu
3. **Mubahu na pia huwa makruhu (haipendelewi kwake ndoa):** Kwa yule asiye na matamanio wala kuelekea katika jambo la ndoa
4. **Haramu:** kwa aliye katika nchi ya kikafiri yenye kuupiga vita uislamu. Sababu kuingia kwake kwenye ndoa, ni kuingiza familia katika kutawaliwa na makafiri na kupelekea kuharibu kizazi na hata mke pia

IDADI YA WAKE ANAORUHUSIWA MWANAUME KUWAOA

Mwanaume katika uislamu ameruhusiwa kuoa mke zaidi ya mmoja na wasiozidi wanne kwa sharti la kufanya uadilifu kwa wakeze na kuaminika kutofanya dhulma. Na uadilifu unaokusudiwa ni kuwafanyia sawa katika malazi, mavazi na maskani. Anasema Allah ﷻ

﴿ فَٱنكِحُواْ مَا طَابَ لَكُم مِّنَ ٱلنِّسَآءِ مَثۡنَىٰ وَثُلَٰثَ وَرُبَٰعَۖ فَإِنۡ خِفۡتُمۡ أَلَّا تَعۡدِلُواْ فَوَٰحِدَةً ﴾ النساء [٣]

Basi oeni wanaopendeza kwenu katika wanawake, wawili wawili, watatu watatu, wanne wanne. Na endapo mkihofia kufanya uadilifu basi oeni mmoja. (Suurat Annisaa, aya 3)

Ama kufanya uadilifu katika kufanya sawa katika mapenzi hili ni jambo ambalo haliwezekani, na hii ndio maana ya kauli ya Allah ﷻ

﴿ وَلَن تَسۡتَطِيعُوٓاْ أَن تَعۡدِلُواْ بَيۡنَ ٱلنِّسَآءِ وَلَوۡ حَرَصۡتُمۡۖ ﴾ النساء [١٢٩]

Na kamwe hamtoweza kufanya uadilifu baina ya wanawake hata kama mtakuwa na pupa katika hilo. (Suurat Annisaa, aya 129)

Makusudio ya uadilifu katika aya hii ni mtu kuweza kuwapenda sawa wake zake. Na hili ni jambo muhali. Anasema Imam Abuu Muhammad, Hussein bin Mas-u'Al-baghawiy katika tafsiri yake

[5] Angalia kitabu Al-mulakhasul-fighiy 2/324 cha Sheikh Fawzaan Al-fawzaan

أَيْ: لَنْ تَقْدِرُوا أَنْ تُسَوُّوا بَيْنَ النِّسَاءِ فِي الْحُبِّ وَمَيْلِ الْقَلْبِ

“Maana yake, hamuwezi kufanya sawa baina ya wanawake katika kuwapenda na kuelekea kwa moyo – kwa kumpenda zaidi mwingine”

Hivyo, inaweza kutokea mtu kumpenda zaidi mmoja katika wake zake kwa sababu miongoni mwa sababu, ila anatakikana kwake kuwafanyia uadilifu katika huduma – chakula, mavazi, na malazi.

Hili linaonesha wazi kuwa, hakuna mke ambaye atakayekuwa na haki pungufu kulinganisha na mwenzake. Hawi mke mdogo ni mwenye kudharaurika, au kuhisi ameingilia ndoa ya mke mwingine, au chaguo la pili n.k. katika maneno yanayoonesha kuwa hastahiki kuolewa katika nafasi hiyo.

Vilevile tunapata faida kuwa, anayeolewa mke wa pili sio mjane pekee, bali hata binti ambaye hakuwahi kuolewa. Ikiwa kigezo cha mume kuongeza mke ni uadilifu, basi hakuna atakayeonewa katika wake, hata kama kuna mizozo itakayojiri baina yao. Na mizozo hiyo kutokea haitegemeani kuwa mwanamke ni wa kwanza au wapili n.k.

<u>HEKIMA YA SHERIA KATIKA UKE WENZA:-</u>

1. Kabla ya Uislamu ilikuwa mwanaume anaoa wanawake anaowataka, kwa idadi aitakayo, pasi na kuchunga kufanya uadilifu baina ya wake zake. Uislamu ukaweka ukomo wa wake wa kuwaoa mwisho wanne, tena kwa kuzingatia kigezo cha uadilifu.

عَنْ عَبْدِ اللهِ بْنِ عُمَرَ، قَالَ: أَسْلَمَ غَيْلَانُ بْنُ سَلَمَةَ وَتَحْتَهُ عَشْرُ نِسْوَةٍ، فَقَالَ لَهُ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم ((خُذْ مِنْهُنَّ أَرْبَعًا))

Amesimulia Abdullah ibn Umar - Allah amridhie- ya kwamba: Alisilimu Ghaylaan bin Salama na akiwa na wake kumi (10), Mtume – juu yake sala na salamu, akamwambia, “Chukua miongoni mwao wanne”[6]

   Hivyo, jambo la kuoa mke zaidi ya mmoja ni jambo la kale. Na ndio maana hata katika miji yetu tunaona machifu walikuwa wakioa wake zaidi ya mmoja. Na mpaka sasa hilo ni jambo endelevu kama inavyoshuudiwa kwa Mfalame wa Eswatini na wengineo katika watu wasiofungamana na mafundisho ya kuwa na mke mmoja tu.
2. Jambo la uke wenza linaendana na maumbile sahihi ya viumbe hai katika wanaadamu na wanyama. Sababu mwanaume mmoja akiwa na mke zaidi ya mmoja, malengo ya kupata watoto wengi yanafikiwa zaidi. Hivyo, mwanaume mmoja anaweza kuwabebesha ujauzito wanawake wengi kwa wakati mmoja. Na

[6] Musnad Ahmad, hadithi na. 5027

hata kwa wafugaji, hupendelea kuwa na majike mengi katika mifugo kuliko madume ili kuweza kupata idadi kubwa ya mifugo n.k.

3. Katika tafiti nyingi zinaonesha kuwa idadi ya wanawake ni kubwa zaidi ya idadi ya wanaume[7]. Hivyo, mwanaume kuwa na mke mmoja tu, ni kuwakosesha wanawake fursa ya kuolewa na kupata mahitajio ya kibinadamu, na kuhifadhi tupu zao kutokana na zinaa.
4. Kimaumbile mwanamke anapitia vipindi kama vya hedhi na nifasi, vipindi ambavyo mwanaume vinampa dhiki katika kukidhi matamanio yake na kupata fursa ya kuwa na watoto wengi anaowahitaji. Jambo ambalo mwanamke matamanio yake si kama ya mwanaume na anaweza kustahimili kupindi kirefu kuliko mwanaume.
5. Mwanamke pia hufikia kipindi cha ukomo wa kuzaa, hivyo mwanaume kuwa na mke zaidi ya mmoja humpa fursa ya kupata idadi ya watoto awahitajio.

Idadi isiyozid wake wa nne ni kwa wanaume wote, isipokuwa Mtume wetu Muhammad ﷺ, yeye hakupewa idadi maalumu, kama alivyobainisha Allah ﷻ

﴿ وَٱمۡرَأَةٗ مُّؤۡمِنَةً إِن وَهَبَتۡ نَفۡسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنۡ أَرَادَ ٱلنَّبِيُّ أَن يَسۡتَنكِحَهَا خَالِصَةٗ لَّكَ مِن دُونِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَۗ قَدۡ عَلِمۡنَا مَا فَرَضۡنَا عَلَيۡهِمۡ فِيٓ أَزۡوَٰجِهِمۡ وَمَا مَلَكَتۡ أَيۡمَٰنُهُمۡ لِكَيۡلَا يَكُونَ عَلَيۡكَ حَرَجٞۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورٗا رَّحِيمٗا ﴾ الأحزاب [٥٠]

Na (tumekuhalishia ewe Mtume) mwanamke muumini endapo akijitoa nafsi yake, ikiwa Nabii akitaka kumuoa, hali ya kuwa ni pekee kwako wewe kinyume na waumini. Kwa hakika tunajua tuliyofaradhisha kwa waumini katika wake zao na wale wawamilikio kwa mkono wa kuume, ili isiwe kwako dhiki. Na Allah ni mwingi wa kusamehe na mwenye huruma. (Suurat Al-ahzaab, aya 50)

<u>MIONGONI MWA HEKIMA ZA MTUME ﷺ KUPEWA UPEKEE WA KUOA ZAIDI YA WAKE WANNE NI KAMA IFUATAVYO</u>:-

1. Ni jambo ambalo ni wahyi, hivyo ni hukumu ya Allah ambayo inahitajika kuchukuliwa kwa dhana njema. Ni kama ambavyo alimpa upekee mambo mengine kamavile: uwajibu wa kusimama usiku, kuunganisha swaumu kwa masiku ayatakayo pasi na kufungua, kutochukua katika mali za sadaka au zaka n.k
2. Katika jambo ambalo linalofahamika ni kuwa, hakuna muadilifu na mwenye tabia njema katika kuishi na wake zaidi ya Mtume ﷺ

وعن عائشة رضي الله عنها قالتْ: قالَ رسولُ الله صلى الله عليه وسلم: ((خيرُكم خيرُكم لأَهْلِه، وأنا خيرُكم لأَهْلي))

Kutoka kwa Mama Aisha -Allah amridhie: amesema Mtume wa Allah ﷺ, “Mbora wenu, ni mbora wenu kwa wake zake, na mimi ni mbora wenu kwa wake zangu”[8]

[7] Angalia Jarida ‘The Economic Survey 2022’, uk. 88 lililotolewa na Wizara ya Fedha, Mwaka 2023
[8] Sahihu Tar-ghiib wa tarhiib, hadithi na. 1924

3. Uwezo wa nguvu alizopewa katika kuudu tendo la ndoa

عن أَنَس بْن مَالِكٍ قَالَ: كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم يَدُورُ عَلَى نِسَائِهِ فِي السَّاعَةِ الْوَاحِدَةِ، مِنَ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ، وَهُنَّ إِحْدَى عَشْرَةَ. قَالَ: قُلْتُ لِأَنَسٍ: أَوَكَانَ يُطِيقُهُ؟ قَالَ: كُنَّا نَتَحَدَّثُ أَنَّهُ أُعْطِيَ قُوَّةَ ثَلَاثِينَ.

Anasimulia Anas ibn malik -Allah amrihie: Alikuwa Nabii ﷺ anazunguka kwa wakeze (katika tendo la ndoa) katika wakati mmoja usiku na mchana, na wao wakiwa wake kumi na moja (11). Akasema Qatadah: Nikasema kumwambia Anas, “Alikuwa anaweza hilo?!” akasema Anas, “Tulikuwa tunasema kwamba, amepewa nguvu za watu thalathini (30)”[9]

4. Mtume ﷺalikuwa akioa kwa maslahi, na si kuangalia matamanion ya nafsi yake, kwa dalili zifuatazo

(i) Kumuoa kwake Mama Khadija – Allah amridhie, akiwa na miaka arobaini (40) na yeye akiwa na umri wa miaka ishirini na tano (25) tu. Kutokuoa mwanamke bikra katika wakeze isipokuwa Mama Aisha – Allah amridhie pekee. Lakini pamoja na kupewa uhuru wa kuoa wake awatakao ila hakuzidisha wake kumi na moja (11)

(ii) Alioa ili wakeze wawe ni walimu kwa wengine kwa yale yaliyokuwa yakitokea katika nyumba yake, katika mambo ambayo umma wahitajia kufahamu. Anasema Allah ﷻ

﴿ وَٱذۡكُرۡنَ مَا يُتۡلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنۡ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ وَٱلۡحِكۡمَةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ٣٤ ﴾ الأحزاب [٣٤]

Na kumbukeni yasomwayo katika majumba yenu katika aya za Allah na hekima (Sunna). Hakika Allah ni mjuzi wa mambo ya siri na mwenye khabari. (Suurat Al-Ahzaab, aya 34)

(iii) Alitumia kama njia ya kulingania. Kwa mfano; alimuoa Juwayriyya binti Al-haarith na ikawa sababu ya kusilimu kabila lake, Banul Mustwaliq

(iv) Alioa ili kuwahifadhi wanawake kulingana na changamoto zao mbalimbali. Alimuoa Ummu Salama, Hindu bint Abii Umayya, ambaye alikuwa ni mwanamke mwenye umri mkubwa na pia alikuwa na watoto. Hivyo alimuoa ili kuwalea watoto na mama yao. Na vilevile alimuoa Sauda bint Zam’ah ambaye Mumewe Sakraan bin Amr alifariki, na wawili hawa walikuwa wamehama kwenda Habasha, hivyo kumuoa kwake Mama Sauda ni kumuhifadhi asirudi kwenye ukafiri endapo akirudi katika Mji wa Makka

(v) Kuwakirimu na kuwatukuza maswahaba zake wakubwa kama alivyomuoa Hafsa Mtoto wa Umar bin Al-kwatwaab, Aisha mtoto wa Abuubakar (Allah awaridhie). Vilevile kuwaozesha maswahaba mabinti zake. Alimuozesha Faatwima kwa Aliy, Ruqayya na Ummu Kuluthum kwa Uthman bin A’ffan

Na mengineyo mengi katika maslahi yaliyofungamana na kuoa kwake. Lakini hili jambo ni katika mambo ambayo Mayahudi na Wakristo walimuonea gere Mtume

[9] Sahih Bukhary, hadithi na. 265

wetu Muhammad ﷺ, na wakusema ikiwa yeye ni Mtume wa kweli kwanini aoe sana? Inaonesha yeye hima yake kubwa ni wanawake!. Allah ﷻ akawajibu ndani ya kitabu chake.

﴿ أَمۡ يَحۡسُدُونَ ٱلنَّاسَ عَلَىٰ مَآ ءَاتَىٰهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضۡلِهِۦۖ فَقَدۡ ءَاتَيۡنَآ ءَالَ إِبۡرَٰهِيمَ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَءَاتَيۡنَٰهُم مُّلۡكًا عَظِيمٗا ٥٤ ﴾

النساء [٥٤]

Hivi (Mayahudi) wanawahusudu watu (Muhammad ﷺ) kwa kile ambacho Allah amewapa katika fadhila zake (katika uhalali wa kuoa wanawake) kwa hakika amewapa watu wa Ibrahim (Daud na Sulayman) Kitabu, na Hikma (Utume), na akawapa Ufalme Mkubwa (wake wengi). (Suurat Annisaa, aya 54)

Wamefasiri hivyo, Ibnu Abbas, Al-hassan, Mujaahid na wengineo kama alivyonukuu Imam Al-baghawiy katika tafsiri yake (Ma'alimu At-tanziil).

Na inasemwa kuwa Sulayman alikuwa na wake elfu moja (1000), mia saba (700) vijakazi na huru mia tatu (300), na Daud alikuwa na wake mia moja (100). Vipi mumtie lawama Nabii Muhammad ﷺ kwa kuoa wake kumi na moja (11)?[10]

NASAHA KWA WASIMAMIZI WA VIJANA WA KIKE NA KIUME

Zifuatazo ni nasaha kwa wasimamizi wa vijana wa kiume na wa kike waliofikia umri wa baleghe

1. Kujitahidi kufuatilia nyenendo za vijana wao katika maisha yao ya kila siku, kwa kuwapa miongozi ya uislamu kunako mahusiano yanayofaa na yasiyofaa, pamoja na kufanya jitihada ya kuwaweka mbali na vishawishi vya kuingia mahusiano ya haramu. Maana hilo ni wajibu kwao kama alivyosema Allah ﷻ

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا ﴾ التحريم [٦]

Enyi Mlioamini! Ziokoeni nafasi zenu na za watu wenu kutokana na moto (Suurat At-tahriim, aya 6)

2. Kuwafanyia wepesi vijana jambo la kuingia katika ndoa. Ikiwa ni kijana wa kiume ambaye umri wa kuoa umefika, basi mlezi wake amsimamie katika kumuozesha kwa kumsaidia mahari na mazingira ya kuweza kumudu ndoa. Na ikiwa ni binti, basi atakapoposwa, wasiweke kizuizi eti kisa anasoma chuo mpaka amalize, kulifanya hilo ni kuchangia vijana wengi kuona ndoa ni kizuizi cha maendeleo yao, na pia kuona zinaa ni kitu cha kawaida sana kwao

﴿ وَأَنكِحُواْ ٱلۡأَيَٰمَىٰ مِنكُمۡ وَٱلصَّٰلِحِينَ مِنۡ عِبَادِكُمۡ وَإِمَآئِكُمۡۚ إِن يَكُونُواْ فُقَرَآءَ يُغۡنِهِمُ ٱللَّهُ مِن فَضۡلِهِۦۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٞ ٣٢ ﴾ النور [٣٢]

Na waozesheni wasio na wenza (mke au mume) miongoni mwenu, na (muwaozeshe) wema katika watumwa na vijakazi. Endapo wakiwa mafukara, basi Allah atawatajirsha kwa fadhila zake. Na Allah ni mwenye wasaa, mwenye elimu (Suurat nuur, aya 32)

[10] Angalia Ma'aalim At-tanziil 1/569 ya Imam Al-baghawiy

HITIMISHO

Baada ya kumaliza sehemu ya kwanza ambayo ni utangulizi wa kuingia katika maudhui ya ndoa, sehemu inayofuatia, sehemu ya pili itajikita katika kubainisha hukumu za posa na uchumba. Hivyo tukae mkao wa kula kupokea mada hiyo na Allah akubarikini.

MAREJEO

- **Vitabu va dini**

Ahmad ibn Hanbali. (1416 H). *Musnadul Imaam Ahmad ibn Hanbali*. Daarul hadith

Albaghawiy. (1420 H). *Maalimu Attanziil*. Daaru Ihyaai turathil A'raby

Albukhary. (1414 H). *Sahiihul Bukhary*. Daaru ibn Kathiir

Jopo la wanazuoni. (1437 H). *Al fiqhul muyassar*. Daarul ghad Al-jadiidu

Muslim ibn Al-hajjaaj. (1374 H). *Sahihu Muslim*. Matba'tu I'isa Alhalaby

Naaswirud diin Al-albaaniy. (1421 H). *Sahiihu Attarqhiib wa Attarhiib*. Maktabatul Maarif

Saalih Al-Fawzan. (1423 H). *Almulakhaswul fiqhiy*. Daarul A'aswima

- **Vitabu visivyo vya dini**

Ministry of Finance (2023), *The economic survey*

Imekusanywa usiku wa Jumaapili, 02 Shawwaal 1447 = 21/03/2026

Zanzibar, Tanzania

+255 772 808 543/ +255 714 036 096